

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 10 The monkey and the tortoise

Author: Ibrahima Ndiaye

## **LEARNING BY EAR 2010**

### **SHALL I TELL YOU SOMETHING? AFRICAN FABLES FOR A CULTURE OF PEACE**

#### **EPISODE 10: „THE MONKEY AND THE TORTOISE“**

**AUTHOR:** IBRAHIMA NDIAYE

**EDITORS:** YANN DURAND, STEFANIE DUCKSTEIN,  
NAÏMA GUIRA

**TRANSLATION:** NATALIE GLANVILLE-WALLIS

**PROOFREADING:** TONY DUNHAM

**KISUAHELI :** ERIC PONDA

**Sound Clips: liegen bis Mitte Juli vor**

#### **CHARACTERS:**

1. NARRATOR (male, 40 years old at least)
2. TORTOISE (female, about 20)
3. MONKEY (male, about 20)
4. ELEPHANT (male, about 40 or older)
5. BUTTERFLY (female, about 20)

## **INTRO / PRESENTER:**

Hujambo msikilizaji na karibu kwa kipindi cha Noa Bongo! Jenga Maisha yako. Hata hivyo tunaanza kwa habari ambazo bila shaka hazitakufurahisha, kwani hiki ni kipindi cha kumi na cha mwisho katika msururu wetu wa vipindi vilivyoangazia hadithi za Afrika kuhusu utamaduni na amani. Hata hivyo usiwe na wasi wasi kwani kwa vile ni kipindi cha mwisho tunatumai kwamba kitakusisimua vilivyo. Na hivi leo tutasikia hadithi kuhusu mzozo baina ya wanyama wawili tofauti kabisa. Mmoja mtundu na mwingine mpole na mwenye bidii sana. Karibu kwenye hadithi ya tumbili na kobe.

### **1. MUSIC (*play as background for the entire script*)**

### **2. NARRATOR:**

Zamani za kale katika shamba la wanyama, palitokea msimu ambao kila mmoja alitaraji kupata mavuno mengi ambavyo haijawahi kushuhudiwa katika historia ya shamba hilo kufuatia msimu uliofana sana mwaka huo.

### **3. SFX: Strikes of a hoe**

### **4. NARRATOR:**

Kobe ambaye alifanya kazi kwa bidii katika shamba lake alipata mavuno mazuri kweli. Alivuna mananasi na viazi vitamu vingi sana. Lakini hata hivyo hakuwa na shukrani.

### **5. TORTOISE (*complaining to herself*):**

“Oh! kama ningepata mahindi pia !...

Yaani angalau mazao ya aina mbali mbali ingekuwa bora zaidi kwangu, lakini sasa inanibidi niende sokoni niuze mali kwa mali ili niweze kupata mahindi.

## 6. NARRATOR:

Huku akiwa amebeba kapu lake zito lililomfanya kusuasua barabarani, na baada ya kutembea mwendo mrefu kwenye jua kali, Kobe alishikwa na kiu. Ghafla akasikia maji yakinirika mtoni, hali iliyozidishia kiu chake.

## 7. SFX: *Swashing water*

## 8. NARRATOR:

Hivyo hakuweza kujizuia, na akaweka kapu lake chini kando ya barabara na kujikokota guu moja guu pili hadi kwenye mto kutafuta maji ya kunywa. Msikilizaji, wajua ni nani aliyepita barabarani wakati Kobe ameacha kapu lake kwenda kutafuta maji? Si mwengine bali tumbili mjanja.

## 9. MONKEY:

“Hahahaha... Hahahaha” (*mischiefous laughing*) “Oh ni bahati iliyojie!”

(*monkey rubbing his hands*)

## 10. NARRATOR:

Tumbili akakukuta mikono yake kwa raha ya kuokota kapu lililoja matunda kando ya barabara. Kisha bila ya kupoteza wakati akalinyakua kapu hilo upesi na kupanda juu ya mti uliokuwa karibu. Kobe aliporudi kutoka mtoni, hakuamini macho yake, kapu lake lilikuwa limetoweke, jambo lililomkasirisha asijue la kufanya.

## 11. TORTOISE (*horrified*):

“Si....si....siamini...!Hai-hai-haiwezekani. Nani amebeba kapu langu. Nimeliacha hapa muda mfupi tu uliopita hivi limetoweke! Mkosi gani huu jamani? Lakini sioni yeoyote karibu na mahali hapa, sasa ni nani anayeweza kuwa ameliiba! Au naota?

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 10 The monkey and the tortoise

Author: Ibrahima Ndiaye

## 12. BUTTERFLY:

“Hiihihi, kweli? Unahakika umeacha kapu la matunda  
mahali hapa?

## 13. NARRATOR:

Mara akatokea kipepeo mdogo ambaye alishuhudia yote  
yaliyotokea.

## 14. TORTOISE:

“Oh kipepeo, mimi sioti. Kwani umemuona nani akipita  
hana?

## 15. BUTTERFLY:

“Hebu tazama pale juuu!

## 16. NARRATOR:

Kobe akatazama juu ya ule mti na hakumini macho yake.  
Tumbili akiwa amekalia tagaa moja alikuwa akila kwa ulafi  
mavuno yake ambayo ameyapata kwa jasho. Tayari  
alikuwa amekula viazi vitamu na nusu ya mumunye.

## 17. TORTOISE (*screaming*):

“Koma unachofanya sasa hivi! Hilo kapu na vyote vilivvomo  
ndani ni vyangu.

## 18. MONKEY (*sniggering*):

“Samahani, sielewi unazungumzia nini. Nimelipata kapu hili  
limeachwa kando kando ya barabara .

## 19. TORTOISE (*shouting exasperated*):

Nimeliacha hapa kapu langu kwenda kutafuta maji ya

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 10 The monkey and the tortoise

Author: Ibrahima Ndiaye

kunywa sababu nilikuwa na kiu sana! Lete kapu langu, la sivyo nitakwenda kukushtaki kwa hakimu Ndovu.

## 20. MONKEY:

"Fanya uwezelo wee. (**keeps on eating, talking on with a mouthful of food**) Naijua sana sheria inasema hivi: yeote atakayeokota chochote barabarani ana uhuru wa kukihifadhi. Kwamba unapookota kitu chochote, basi hiyo inakuwa ni mali yako, ndio maana yake.... !Yaani kihifadhi unachookota!"

## 21. NARRATOR:

Baada ya kuambiwa maneno hayo ya jeuri, Kobe akaanza kuwaza. Akawaza mpaka akashikwa na jazba, jasho likaanza kumtiririka mwilini. Jioni akaenda kumuona Ndovu na kumueleza tetesi zake huku akishinikiza haki itendeke. Kipepeo na Mjusi pia waliandamana naye kama mashahidi wawili waliokuwepo wakati kisa hicho kikitokea. Tumbili pia alifika kwa hakimu na jeuri zake!

## 22. MONKEY:

"Hapa hakuna kesi. Kapu lilikuwa limeachwa barabarani. Nikalichukua na kulihifadhi. Je, kuna makosa? Kulingana na sheria za hapa, mtu anapaswa kuhifadhi chochote anachokiokota. Yaani hifadhi unachookota, si ni kweli hakimu Ndovu?"

## 23. ELEPHANT:

"Hmmmmm (**thinking**). Samahani lakini nakubaliana na Tumbili. Katika kisa hiki mali inayookotwa bila shaka ni mali ya mwenye kuokota. Niwie radhi Kobe, najua ulijitahidi sana na kujikakamua kupata mavuno haya mazuri, lakini sasa Tumbili ana haki ya kubaki na kapu na

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 10 The monkey and the tortoise

Author: Ibrahima Ndiaye

vyote vilivyoko ndani."

## 24. MONKEY *shouts for joy + hysterical cries*

## 25. NARRATOR:

Kobe alishtushwa na uamuzi huo akiwa na machungu tele. Lakini baada ya muda alichangamka na akaamua kumtembelea dadake, kwa matumaini kwamba huenda amebakisha mahindi kidogo amsaidie. Hivyo asubuhi ilipofika, akafunga safari kwenda kwa dadake. Baada ya kutembea kwa mwendo mrefu huku juu kali likiwa linawaka, ghafla alimuona yule Tumbili amelala usingizi mzito kando ya barabara akiwa na yale mananasi, mamumunya na viazi vitamu, huku mkia ameunyoosha.

## 26. MONKEY: *snoring noises*

## 27. NARRATOR :

Nusura kobe azimie, kwa furaha ya kumuona Tumbili. Na bila ya kusita aliung'ata mkia wa tumbili na hakuachilia tena. Huyo akaanza kutoroka.

## 28. TORTOISE (*whispering to herself*):

"Leo, nitamfunza sheria na jinsi inavyofanya kazi!"

## 29. MONKEY (*panic cries*):

"Jamani! Nisaidieni, mshikeni mwizi, mzuieni! Wewe unafanya nini na mkia wangu?"

## 30. NARRATOR:

Kobe akanyamaza, hakutaka kufungua mdomo wake kwani angefanya hivyo ule mkia wa Tumbili ungemponyoka.

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 10 The monkey and the tortoise

Author: Ibrahima Ndiaye

Lakini Kipepeo aliyejekuwa akipita akamuona na kupiga makelele kutoka juu.

### **31. BUTTERFLY (*laughing*):**

"Tumbili, nadhani Kobe ameokota mkia wako barabarani na ameamua kuuhifadhi! Oh, hebu tazama anayekuja... Ni hakimu, ndovu!"

### **32. ELEPHANT: *roars sounds***

### **33. ELEPHANT:**

"Ni kweli kipepeo..... ! Bila shaka Tumbili una uhuru wa kupeleka kesi hii mahakamani. Hata hivyo lakini naona itakuwa kazi bure tu, kwani sheria ya Savanna inatumika hapa pia kama ilivyotumika katika kesi ya kapu la Kobe: Mtu anapasa kuhifadhi anachookota. Yaani hifadhi unachookota. Sasa Kobe unaweza kwenda na mkia wa Tumbili pengine utakusaidia kufukuza nao nzi."

### **34. MONKEY (*panic cries*):**

"Hapana, eti aende na mkia wangu huu mzuri kufukuzia nao nzi? Hapana haiwezekani! Tafadhali nurudishie mkia wangu na mimi nitakurejeshea kapu lako la matunda na juu yake nitakupa kapu jingine la viazi vitamu kama fidia."

### **35. ELEPHANT:**

"Hiyo haitoshi kurejeshewa mkia wako. Je unakubali na kuniahadi kurejesha kapu hilo na gunia jingine la viazi vitamu na mahindi kesho asubuhi ?.

### **36. NARRATOR:**

Japo alikuwa amekasirika, ilimbidi Tumbili akubali. Naye Kobe akiwa na furaha kubwa aliuachilia mkia wa Tumbili na

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 10 The monkey and the tortoise

Author: Ibrahima Ndiaye

kumshukuru sana hakimu Ndovu. Kisha hao kila mmoja akashika njia kwenda zake nyumbani akiwa ameridhika. Siku hiyo jioni alikula mamumunya na viazi vitamu na kulala. Kobe alikifurahia sana chakula hicho huku akiridhika kwamba haki imetendeka.

*Na hadi hapo ngano yetu inafika ukingoni, na wa kwanza kuvuta harufu yake, bila shaka ataiona mbingu.*

## 37. Music

### **OUTRO / PRESENTER:**

Bila shaka Tumbili mjanja alistahili uamuzi huo, ama? Na hii inatufunza kwamba mizozo inaweza kutatuliwa kwa kitumia hekima bila ya kumdhuru yeyote.

Hivyo basi Kobe mwaminifu na mwenye bidii alipata haki na mwisho wake ukawa mwema. Hadithi yetu ya Tumbili na Kobe ndio inayotukamilishia msururu wa ngano zetu

Learning by Ear 2010

Series: Shall I tell you something? African Fables for a culture of peace

Episode: 10 The monkey and the tortoise

Author: Ibrahima Ndiaye

kuhusu utamaduni wa Mwafrika katika kuleta amani na maridhiano mionganini mwa jamii. Ngano hizi zimeandikwa na Ibrahima Ndiaye kutoka nchini Senegal.

Alituelieza kwamba alisimuliwa ngano hizi na bibi yake kitambo kidogo. Ngano ambazo pia yeye huzisimulia watu wengine kwa manufaa ya jamii. Endapo umekosa kusikiliza hadhithi yoyote ama ungependa kusilikiza tena ngano hizi, tembelea mtandao wetu wa: [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe).

Je, una maoni gani kuhusu hadithi hizi ? Na Je, unadhani zinaweza kusaidia katika kutatua au kuzuia mizozo mionganini mwa jamii?

Tutafurahi sana kupokea maoni yako msikilizaji kupitia email : [lbe@dw-world.de](mailto:lbe@dw-world.de)

Huku tukiwa na wingi wa matumaini kwamba umefurahia hadithi hizi na utajumuika nasi tena katika msusuru wa hadithi zetu nyingine za Noa Bongo. Shukran sana na kwaheri kwa sasa.

..... ENDS.....